# Ni nini UKIMWI?

HIV ni virusi vinavyosababisha UKIMWI. Kwa muda virusi hivi (HIV) hudhobisha mwili wako na kuufanya ushindwe kupambana na magonjwa. Mtu anapokuwa mgonjwa sana kutokana na HIV anaweza kuwa na UKIMWI.

## Vipi mtu huambukizwa virusi vya UKIMWI?

Wengi wa akina mama walio na virusi vya UKIMWI waliambukizwa kutokana na kufanya mapenzi na wanaume bila ya kujikinga. Bila ya kupimwa hakuna jinzi ya kujua kama mtu anayo UKIMWI ama haana. Kwa hivyo mwanamke anaweza kuambukizwa na virusi vya UKIMWI bila ya kujua hata kama alikuwa na mpenzi mmoja tu.

Mwanamke anaweza pia kuambukizwa virusi vya UKIMWI kwa kutumia sindano au vifaa vingine vya kujidunga dawa pamoja na mtu mwengine mwenye virusi vya UKIMWI.

## Kwa wanawake wasiopimwa virusi vya UKIMWI

Katika mwaka 1998 Wizara ya Afya ilianzisha mpango wa kupima UKIMWI wajawazito na kushauri wahudumu wa afya kujadiliana na kuwafanyia vipimo vya UKIMWI akina mama wajawazito wote na wale wanaopanga mimba. Damu unayobakia ambayo kwa kawaida ingemwagwa, ingeweza kutumika kwa uchunguzi ili kuona kiasi cha maambukizo ya UKIMWI kwa akina mama katika Ontario. Hivyo basi habari zote za utambulisho (kama vile jina, nambari ya kadi ya afya) zitatolewa kabisa na hutapewa (wala hutaweza kupewa) majibu. Kama hupendi damu yako itumike katika utafiti tafadhali mwambie daktari wako.

# Kwa habari zaidi piga simu:

Simu ya UKIMWI ya Ontário 1-800-668-2437
(Kingereza na lugha nyengine 15)
1-800-267-7432 (Kifaransa)

INFOline 1-877-234-4343
TTY 1-800-387-5559

Simu ya afya ya Hatari za Maambukisi ya UKIMWI kwa mama / Motherisk HIV Healthline
1-888-246-5840

Daktari wako au kituo cha afya ya jamii mtaani kwako

Jumuia ya huduma za UKIMWI mtaani kwako

www.health.gov.on.ca
www.HealthyOntario.com

Msaada wa fedha kutoka wizara ya afya ya Canada.

Catalogue 7610-6133681 Revised 5M June/06 ISBN 0-7794-2254-6 © Queen's Printer for Ontario, 2003

Mpango wa kupima ukimwi katika uja uzito



# Kupimwa UKIMWI ni muhimu kwako na kwa mtoto wako.

Ontario
Ikiwa Bado Mapema

# Kwa nini nifikirie kuhusu kupimwa UKIMWI sasa?

Kipimo cha UKIMWI mapema katika mimba yako kitakupa habari zitakazokusaidia kufanya uamuzi bora na wa dhamana kuhusu afya yako na ile ya mtoto wako.

Zaidi ya vipimo vya damu vinavyohitajika kufanywa katika ujauzito wako, daktari wako au mkunga hushauri kwamba wajawazito wote wapimwe UKIMWI. Unaweza pia kumuhusisha mushirika wako kuhusu UKIMWI.

## Kipimo cha UKIMWI

Kipimo cha UKIMWI ni sahihi na hakina gharama yoyote. Kipimo kinaweza kuagizwa pamoja na vipimo vingine vya ujauzito. Pia kinaweza kupimwa pamoja na vipimo vya damu vya ujauzito.

Ni lazima kupimwa kama upo mjamzito ama unategemea kuwa mjamzito.

Kama unayo niya ya kupumiwa UKIMWI mueleze muhudumu wa afya atakujibu maswali yote ambayo unayo.

Muhudumu wako wa afya hawezi kuagiza kipimo cha UKIMWI bila idhini yako. Na kama ukiamua kwamba hutaki kupimwa, muhudumu wako ataendelea kukupa huduma kama anavyohudumia wagonjwa wengine.

## Majibu ya kipimo

Ikiwa kipimo kitaonyesha **ahuna** UKIMWI inamaanisha kwamba hujaambukizwa. Hata hivyo kama ulijihatarisha na UKIMWI karibuni, kama kufanya mapenzi bila kinga au kutumia pamoja na watu wengine sindano au vifaa vyengine vya kundungia **basi ni vizuri ufikirie kupima** tena katika miezi mitatu.

Ikiwa kipimo kitaonyesha kama una UKIMWI inamahanisha kwamba umeambukizwa na unaweza pia kumuambukiza mtoto wako bila ya kujua, katika ujauzito, wakati wa uchungu, kujifungua na kwa kunyonyesha. Hata hivo kuna matibabu ya kufaa na misaada kukuwezesha uendelee na afya na kupunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa kumuambukiza virusi mtoto wako.

Kama inavyotokea kwa magonjwa mengine mengi, majibu ya vipimo huchukuliwa na Wizara ya afya. Tazama orotha za kipimo cha siri.

**Haya ni baadhi ya maswali unayoweza kuwa nayo kuhusu kipimo cha UKIMWI, itakusaidia kuchukua uamuzi sahihi.**

*Nina uhakika sina ukimwi kwa nini nipimwe?*

Ni muhimu kuwa na uhakika. Ndio maana kipimo cha UKIMWI na ujauzito (hepatitis B, rubella na syphilis) inafanywa kwa kuambatana.

*Jee ni lazima kupimwa sasa ama nitafikiria kuhusu kupimwa?*

Ikiwa unataka kuchukua muda wa kufikiria kwa maelezo uliyopata kwa muhudumu, unaweza kusubiri kupimwa. Ikiwa umeamua kupimwa UKIMWI baadaye, kumbuka kuuliza upimwe katika kipimo cha ujauzito ifuatoyo na kuomba majibu kwa muda wa wiki mbili baada ya kipimo ama unaweza kupanga kupimwa sehemu nyingine kama vile vipimo vya UKIMWI vya siri.

*Ni muda gani inachukua kwa mimi kupata majibu ya kipimo?*

Inachukua muda wa wiki mbili kupata majibu ya kipimo. Kwa wakati huo unasubiri, kama unakabiliwa na shida kama akina mama wengine, tunakuomba uzungumze na mshauri ama mtoaji huduma za afya mtaani kwako kuzungumza swala lako.

*Nitafanya je kama nina UKIMWI? Na mwanangu je?*

Madawa kadhaa huboresha afya za watu wenye UKIMWI na kuwasaidia kuishi muda mrefu zaidi. Baadhi ya madawa haya yameonyesha kupunguza uwezekano wa kumwambakiza virusi mtoto wako kwa asilimia moja mpaka mbili. Bila matibabu kuna uwezekano asilimia 15 mpaka 30 kuamba utamuambukiza virusi mtoto wako. Uzazi wa kupasuliwa vilevile unaweza kupungua uwezekano wa kuambukiza virusi mtoto wako wakati wa kujifungua.

*Kama nina UKIMWI jee niendelee na ujauzito?*

Unaweza kupata matibabu na misaada uendelee na afya katika ujauzito wako na kupungua uwezekano wa kumuambukiza virusi mtoto wako. Unaweza kujadiliana na muhudumu wako wa afya juu ya njia nyengine.

*Vipi nitamueleza mshirika wangu?*

Kuelezana habari ni vigumu na inategemea kwa kiasi juu ya aina gani ya uhusiano unao pamoja na mshirika wako. Kuna washauri-nasaha wenye upendo na watoaji huduma za afya wenye upendo wanaoweza kukusaidia kufanya mpango na pia kukusaidia kuutekeleza. Anza kwa kumuomba muhudumu wako wa afya msaada.

*Kipimo kikionyesha kama ninayo UKIMWI, inaweza kudhuru uamiaji ama usafiri wangu?*

Kipimo kikionyesha umeambukizwa vilevile itaweza kumaanisha kwamba mipango yako ya kuhama au kusafiri kupata kwako bima ya maisha na uhusioano wako yanaweza kuhadhiriwa.

## Vipimo vya UKIMWI vya siri

Ikiwa una shaka juu ya jina lako kutumiwa katika kipimo cha virusi vya UKIMWI unaweza kupimwa kati ya vituo vya kupimia UKIMWI vyenye siri katika Ontario. Hii ina maana kwamba majibu ya kipimo chako hayafahamiki na mtu yeyote mpaka umwambie. Muhudumu wako wa afya hawezi kukupatia kipimo cha UKIMWI cha siri. Ni baadhi tu ya vituo vya afya vilivyoteuliwa kupima ukimwi vya siri.

# Vipimo vya UKIMWI vya siri ya Ontario

| | |
|---|---|
| Algoma Health Unit | 705-541-7100 |
| Anishnawbe Health Toronto | 416-360-0486 |
| Bay Centre for Birth Control, Women's College Hospital | 416-351-3700 |
| Birth Control & Venereal Disease Information Centre | 416-789-4541 |
| Central Toronto Community Health Centres | 416-703-8482 |
| Centre francophone de Toronto | 416-922-2672 |
| Centretown Community Health Centre | 613-563-2437 |
| City of Hamilton Public Health and Community Services Department | 905-528-5894 |
| Toronto Public Health | 416-338-7600 |
| Elgin-St. Thomas Health Unit | 519-631-9971 |
| Hassle Free Clinic, Women's clinic:<br>Men's clinic: | 416-922-0566<br>416-922-0603 |
| Kingston, Frontenac and Lennox and Addington Health Unit | 613-549-1232 |
| London InterCommunity Health Centre | 519-673-4427 |
| Ottawa Public Health Department | 613-563-2437 |
| Peel Health Department | 905-799-7700 |
| Region of Waterloo Public Health | 519-883-2251 |
| Regional Niagara Public Health Department | 905-688-3817 |
| Rexdale Community Health Centre | 416-744-0066 |
| Sandy Hill Community Health Centre | 613-563-2437 |
| Simcoe Muskoka District Health Unit | 705-721-7520 |
| Somerset West Community Health Centre | 613-563-2437 |
| Sudbury and District Health Unit | 705-522-9200 |
| Thunder Bay District Health Unit | 807-625-5981 |
| Wellington-Dufferin-Guelph Health Unit | 519-821-2370 ext. 2235 |
| Windsor-Essex County Health Unit | 519-258-2146 |
| Windsor Regional Hospital, Metropolitan Campus | 519-254-6115 |